



## Maswali na Majibu

1. Mbona Mungu aliwaadhibu watu wa Israeli?  
*Kwa sababu walikuwa waovu na walikataa kutii amri za Mungu.*
2. Watu wa Israeli waliadhibiwa namna gani?  
*Waashuru waliwapiga na kuwachukua mateka.*
3. Ufalme wa Yuda ulikaa kwa miaka mingapi baada ya Waisraeli kushindwa?  
*Zaidi ya miaka 100*
4. Nani alikuwa mfalme wa mwisho wa Yuda? *Sedekia*
5. Mbona Mungu aliadhibu ufalme wa Yuda?  
*Kwa sababu walikuwa waovu na wakakataa kutii amri za Mungu.*
6. Watu wa Yuda waliadhibiwa namna gani?  
*Wakaldayo waliwapiga na kuwachukua mateka.*
7. Mungu aliahidi Daudi nini kuhusu ufalme wake?  
*Ufalme wake utadumu milele. Mwanawe mmoja ataendelea kuwa mfalme.*
8. Mungu atawekaje hii ahadi kwa sababu ufalme uliharibiwa – watu walihamishwa na hakukuwa na mfame tena?  
*Mungu alipindua ufalme MPAKA aliyejaki – Yesu – aje. Mungu atampa taji na atatawala milele.*
9. Mungu aliwapa ahadi gani kabla ya kuchukuliwa mateka?  
*Baada ya miaka 70 watarudi kwa nchi yao.*
10. Wayahudi walirudi lakini hawakuwa na mfalme. Ufalme gani uliwatawala?  
*Ufalme wa Uajemi, ufalme wa Kiyunani na ufalme wa Kirumi.*

## Mistari ya kukariri

Ezekieli 21:25 – 27 Yeremia 29:10

## Mazungumzo

Soma 2 Samweli 7:13 – 16, Ezekieli 21:25 – 27 na Luka 1:30 – 33. Zungumza vile Mungu atatimiza ahadi zake hata kama uovu wa binadamu unaharibu mipango zake

## Kuandika

Soma Yeremia 39:1 – 14. Eleza kuchukuliwa kwa Yerusalem. Waliwazunguka kwa muda gani. Mfalme Sedekia alifanyiwa nini? Nini ilifanyika kwa Yeremia?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 27 Kuchukuliwa mateka na kurudi


**SOMA 2 Wafalme 17:5 – 14; 24:17 – 20; 25:1 – 10; Ezekieli 21:25 – 27**

### SOMO

Mungu alipenda watu wa Yuda na Israeli. Walikuwa ni watu wake wa kipekee. Mungu aliahidi kuwalinda na kuwabariki kwa nchi yao ikiwa watampenda na kumtii. Lakini wasipomtii na waabudu sanamu, angewaruhusu maadui wawapige na kuwachukua mateka kwa nchi yao.

Mungu alifanya iwezekanavyo kuwasaidia watu hawa wampende na kumtii. Aliwapa sheria ili wajue vile wanamtii. Aliwapa wafalme wawaongoze na kuwatawala wakitumia hizo sheria. Aliwapa makuhani wawafundishe sheria za Mungu na kuwasaidia wamwabudie Hekaluni. Tena aliwatumia manabii kuleta ujumbe kwa wafalme na kwa watu.


Wafalme wa kaskazini wa Ufalme wa Israeli walikuwa waovu. Waliongoza watu kuabudu sanamu na kutotii Mungu. Mungu alikuwa mvumilivu sana kwa watu wa Israeli. Alisubiri kwa miaka 200 kusudi hawa watu watubu na wamrudie. Alituma manabii wakiwaonya wakiwambia kwamba wasipobadilika na watubu atawaadhibu. Lakini hawakumsikiliza. Kwa hivyo Mungu aliwaadhibu kwa kuwaachilia wachukuliwe mateka kutoka kwa nchi yao.



Taifa kubwa la nguvu liitwalo Ashuru lilipanua ufalme wake kwa kushinda falme zote zilizokuwa karibu nao. Mfalme wa Ashuru alishambulia Israeli na akashinda. Aliwachukua watu kutoka kwa nchi yenye Mungu alikuwa amewapa. Walichukuliwa kama watumwa na mateka ili waende kuishi kwa nchi ya Ashuru. Hawa watu waliadhibiwa kwa sababu walikataa kutii Mungu na kuvunja ahadi walijomuahidi. Mungu alikuwa amewapa onyo kwamba watachukuliwa mateka ikiwa hawatamtii na kawaida Mungu hutimiza ahadi zake.

Ufalme wa Yuda uliokuwa kusini, ulikuwa na wafalme wengine wazuri. Walimpenda na kumtii Mungu. Baada ya watu wa Israeli kuchukuliwa mateka, watu wa Yuda walikaa zaidi ya miaka 100. Lakini nao pia walikuwa na wafalme wengine waovu. Mungu aliwatumia manabii kuwageuze wamrudie Mungu. Lakini hawakusikiliza. Mwisho watu wa Yuda walikuwa waovu mpaka Mungu akawaadhibu. Sedekia alikuwa mfalme wa mwisho wa Yuda. Alikuwa mfalme dhaifu. Mungu alituma nabii Yeremia kwa Sedekia na kwa watu wake wamrudie na wamtii. Lakini Sedekia na watu wake hawakusikia.

Ufalme wa Ashuru ulishindwa na mfalme wa Babeli. Wakaldayo walikuwa na nguvu zaidi na taifa lao likawashida Waashuru. Nebukadreza, mfalme wa Babeli alishambulia ufalme wa Yuda. Akachukua Yerusalem. Akavunja kuta na kuchoma hekalu pamoja na mji wote. Nebukadreza alichukua Sedekia na watu



Mungu aliahidi Daudi kwamba ufalme wake utadumu milele. Mungu aliahidi kwamba uzao wa Daudi utakuwa ukitawala juu ya huo ufalme. Lakini ufalme huo uliharibiwa. Hakukuwa na mfalme. Watu walichukuliwa mateka kwa nchi zingine. Kwa hivyo ahadi ya Mungu iliisha? Hapani! Mungu hutimiza ahadi yake. Watu wa Mungu walishindwa kutimiza agano (ahadi) na Mungu. Lakini Mungu alipeana njia nydingine ya kutimiza ahadi yake.

Mungu alituma nabii Ezekieli na ujumbe kwa Sedekia, mfalme wa mwisho wa Yuda. Huu ujumbe tunausoma kwa Ezekieli 21:25 – 27. Mungu alimwambia Sedekia kwamba uovu wa Yuda ni kubwa mno na atatoa taji ya utawala kutoka kwa wafalme wa Yuda. Mungu atapindua huo ufalme wenye alisimamisha. Ufalme hautakuweko tena MPAKA aje mtu aliyehaki ndiye atakayetawala watu wa Mungu kwa haki. Hapo ndipo Mungu atampa yule mtu taji. Kwa huu unabii tunaona vile Mungu anatimiza ahadi zake hata watu wakijaribu kuharibu mipango zake.

Ufalme hautaharibiwa kabisa. Mungu ataongoja mpaka mfalme aliyehaki atakapokuja. Yesu ndiye yule aliyehaki. Aliishi maishi kamili. Yeye ni mzao wa Daudi, mfalme wa Israeli. Mungu ameongoja atimize ahadi zake. Hivi karibuni Yesu atakuja kuwa mfalme wa ulimwengu wote milele. Mungu atampa yeye taji. Hapo ahadi za Mungu zitatimizwa.

Kabla watu wa Yuda kwenda matekani, Mungu alikuwa akituma manabii na ahadi ya tumaini. Manabii waliwambia kwamba watakuja kurudi kwa nchi yao. Mungu alisema watakuwa mateka kwa nchi ya Babeli kwa miaka 70. Halafu Mungu atawarudisha kwa nchi yao aliyowaahidi. Watajenga Yerusalem na hekalu.

Baada ya miaka 70, taifa la Babeli lilishambuliwa na kushindwa na Wamedi na Waajemi. Mfalme wa Uajemi aliitwa Koreshi. Koreshi aliweka sheria kwamba watu wote waliomatekani, wanaweza kurudi kwa nchi yao na wajenge hekalu yao. Baada ya miaka 70 mfalme Nebukadreza alipochukua watu wa Yuda, walipata nafasi ya kurudi kwao Israeli. Watu walijenga hekalu na kuta za Yerusalem. Ahadi ya Mungu ilitimizwa kikamilifu.

Mungu alikubali watu wake kurudi kwa nchi yao. Lakini hawakukuwa na ufalme tena. Mungu alikuwa amewanyan'ganya taji kwa kuwa hakukuwa na mfalme. Waisraeli au Wayahudi vile walikuwa wakiitwa, walishi kwa nchi yao kwa miaka 500. Wakati wote walitawaliwa na falme zilizokuwa na nguvu. Hawakuwa na mfalme wa kwao. Kwanza ufalme wa Uajemi, halafu ufalme wa Kiyunani na mwisho ufalme wa Kirumi uliwatawala. Wayahudi waliendelea kungoja mfalme kutoka kwa uzao wa Daudi atakayekuwatoa kutoka kwa ufalme wa Warumi.